

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MUHEZA (MUHEZA WSSA) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-041-2018/2019

Mnamo tarehe 25 Februari 2019 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Muheza (Muheza WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake kwa kipindi cha 2019/20 - 2021/22. Majedwali namba 1-5 yanaonesha mchanganuo wa bei na ada za sasa zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Kiwango cha Matumizi	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
		2018/19	Mabadi liko	2019/20	Mabadi liko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	0-10	450	209%	1,390	1%	1,410	3%	1,450
	>10	495	209%	1,530	1%	1,550	3%	1,590
Biashara	>10	510	208%	1,570	5%	1,650	3%	1,700
Taasisi	>10	500	208%	1,540	1%	1,560	4%	1,620
Viwanda	>10	500	240%	1,700	1%	1,720	3%	1,770
Magati		500	200%	1,500	0%	1,500	0%	1,500

Jedwali 2: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Wateja Wasio na Dira (Shilingi/mwezi)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	4,500	240%	15,300	NA	NA	NA	NA
Taasisi	9,500	197%	28,260	NA	NA	NA	NA
Biashara	10,000	208%	30,800	NA	NA	NA	NA
Viwanda	13,000	227%	42,500	NA	NA	NA	NA

Jedwali 3: Tozo za Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Mwezi).

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo zilizopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	500	NA	0	NA	0	NA	0
Taasisi	500	NA	0	NA	0	NA	0
Biashara	500	NA	0	NA	0	NA	0
Viwanda	500	NA	0	NA	0	NA	0

Jedwali 4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuunganishiwa Maji (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	160,000	Asilimia Ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2013		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				

Jedwali 5: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	10,000	0%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	10,000	50%	15,000	0%	15,000	0%	15,000
Biashara	10,000	50%	15,000	0%	15,000	0%	15,000
Viwanda	10,000	50%	15,000	0%	15,000	0%	15,000

Sababu kuu zilizopelekea kuomba mabadiliko ya bei kama ilivyoielezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Muheza ni kuzalisha mapato ya kutosha ili kukidhi gharama zilizoongezeka za uendeshaji na matengenezo, kuboresha huduma za majisafi, ikiwa ni pamoja na upanuzi wa mtandao na kufanya uwekezaji mdogo, hivyo kuhakikisha huduma bora kwa wateja.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (EWURA Act) Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Ijumaa, tarehe 3 Mei 2019 katika ukumbi wa Tareku uliopo Muheza Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali; Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA; wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Muheza na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha

hapo juu ifikapo tarehe 10 Mei 2019. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **OFISI ZA EWURA KANDA YA KASKAZINI, GHOROFA YA PILI, JENGO LA PPF PLAZA; LINALOFUATANA NA HOTELI YA KIBO PALACE, ENEO LA CORRIDOR au OFISI ZA MUHEZA WSSA ZILIZOPO MJINI MUHEZA.**

Imetolewa na:

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

10 APRILI 2019